Kifurushi cha Taarifa kuhusu Usalama Barabarani

# Mpango wa MiCare wa Funguo za Usalama (Keys to Safety) wa 2026




## Utangulizi kutoka MiCare

Kifurushi hiki cha taarifa kimeandaliwa na MiCare kwa ajili ya washiriki wa mpango wa Funguo za Usalama katika wa mwaka 2026. Tumekusanya taarifa muhimu kutoka kwenye warsha zilizoandaliwa na baadhi ya washirika wetu. Ni sahihi kufikia Juni 2026.

Tafadhali fahamu kwamba hakuna taarifa yoyote katika kifurushi hiki inayoweza kuchukuliwa kuwa ni ushauri wa kisheria. Tafadhali wasiliana na shirika husika ili kujadili hali yako, ikihitajika.

Tunapenda kuishukuru Tume ya Ajali za Usafirishaji (TAC) iliyofadhili mpango huu wa ‘Funguo za Usalama’. Pia tungependa kuwashukuru watoa huduma wote waliofanya mawasilisho na kuendesha warsha, pamoja na wakufunzi wa uendeshaji wa gari kwa ajili ya mpango huu. Tunatoa shukrani zetu pia kwa washiriki wote, kwa ushiriki wenu na shauku yenu ya kujifunza kuhusu usalama barabarani.

## Muhtasari


- **Hatari za kawaida za usalama barabarani**
  Tume ya Ajali za Usafirishaji
- **Gharama ya kumiliki gari**
- **Usajili na uhalali wa gari barabarani**
  Huduma ya Kisheria ya South-East Monash
- **Kupanga kuhusu leseni yako**
  Huduma ya Kisheria ya South-East Monash
- **Kuendesha gari kwa usalama katika Victoria**
  West Justice
- **Kuelewa Bima**
  West Justice
- **Usalama wa kiti cha gari cha mtoto**
  Kuanza Usalama
- **Usiwaache kamwe watoto peke yao ndani ya gari**
  Kuanza usalama


## Tume ya Ajali za Usafiri - Hatari za kawaida za usalama barabarani

### Uchovu

Uwezekano wa kuhusika katika ajali huongezeka sana unapokuwa unasinzia muda kidogo.

Kwa mfano, ukilinganisha na hali ya kulala kwa saa 8, iwapo umelala chini ya saa 5, una uwezekano mkubwa mara nne wa kuhusika katika ajali.

**Mambo unayoweza kufanya kabla ya kuendesha gari:**

- Pata usingizi mzuri wa usiku—ikiwezekana saa nane za usingizi mzuri usioingiliwa—na uepuke kuendesha gari nyakati ambazo kwa kawaida huwa umelala.
- Ikiwa umekosa usingizi au umechoka sana, acha kuendesha gari hadi upumzike vizuri au chukua usafiri mbadala, kama vile usafiri wa umma, teksi au usafiri wa kuchangia na wngine.
- Kwa safari ndefu, panga kupumzika kila baada ya saa mbili za kuendesha gari na ubadilishane kuendesha na mtu mwingine ikiwa inawezekana.
- Ukihisi uchovu unapoendesha gari au ukiona dalili za onyo kama vile kupiga miayo mfululizo, gari kutoka kwenye njia yake, kushindwa kukazia fikira na/au kushindwa kuweka macho wazi, simamisha gari pembeni kwa usalama, lala kwa muda mfupi wa dakika 15 hadi 20, na unywe kahawa au kinywaji chenye kafeini.

## Kuendesha kwa kasi kupita kiasi

Kuendesha gari kwa kasi inayozidi kikomo kilichowekwa ni mojawapo ya sababu kuu za ajali mbaya.

Hata kuzidi kikomo cha mwendo kwa kilomita chache tu kwa saa huongeza sana uwezekano wa kuhusika katika ajali mbaya.

Unaposafiri kwa kasi zaidi una muda mfupi wa kuchukua hatua kisha kushika breki na kusimama ikiwa kuna kitu kitaenda vibaya. Kwa hivyo, kuendesha gari kwa kasi inayozidi kikomo kilichowekwa huongeza uwezekano wa kupata ajali.

Kuendesha gari kwa kasi inayozidi kikomo pia hufanya ajali yenyewe kuwa mbaya zaidi.

Polisi wa Victoria na maelfu ya kamera za usalama barabarani husimamia utekelezaji wa kikomo cha mwendo kasi sehemu zote katika Victoria. Ukiendesha gari kwa kasi inayozidi kikomo kilichowekwa, kuna uwezekano mkubwa wa kukamatwa.

### Unachoweza kufanya

- Hakikisha unaendesha gari ndani ya kikomo cha kasi wakati wote.
- Pia hakikisha unaendesha gari hadi hali itakapobadilika, hii inajumuisha lakini sio tu kupunguza mwendo wako kwenye barabara nyembamba, katika hali ya mvua au barafu, na wakati hakuna mwonekano mzuri.




## Kuendesha Gari Ukiwa Umelewa

Kuendesha gari ukiwa umelewa ni chanzo kinachochangia kwa majeraha ya barabarani ya kuendelea. Kuendesha gari ukiwa umekunywa pombe huathiri mtazamo, maono, umakini, muda wa athari na husababisha usingizi, yote ambayo huongeza hatari ya ajali.

Madereva (na waendesha pikipiki) wenye leseni kamili watakaokutwa wakiendesha wakiwa na kiwango cha pombe katika damu (BAC) cha 0.05 au zaidi hukabiliwa na adhabu kali.

Wanafunzi na madereva wa majaribio lazima wawe na BAC 0.00 (hakuna pombe mwilini mwao).

Polisi wa Victoria hufanya mamilioni ya vipimo vya bila kutazamia vya pumzi kila mwaka. Ukikamatwa na kiwango cha pombe mwilini (BAC) kisichoruhusiwa kisheria, adhabu zake ni kali sana:

Kwa kiwango cha chini, adhabu ni kupoteza leseni kwa miezi 3 na faini, utahitaji pia kukamilisha programu ya mabadiliko ya tabia, kufunga gari lako kwa gharama yako mwenyewe na kuwa na sharti la 0.00 BAC kwa miaka 3.

Ni vigumu sana kujua wakati ambapo kiwango cha alkoholi mwilini (BAC) kiko katika, kimezidi, au kiko chini ya 0.05. Njia pekee ya kuwa na uhakika kwamba uko chini ya kiwango cha kisheria ni kutochanganya kabisa unywaji na uendeshaji gari.

### Unachoweza kufanya

Ikiwa unapanga kunywa pombe, usiendelee kuendesha gari.

Ikiwa unakunywa pombe, tumia usafiri wa umma, teksi au huduma za usafiri na watu wengine. Unaweza pia kupanga kuwa na dereva maalum (yaani, mtu ambaye hanywi pombe na anaweza kuendesha gari).

## Kuendesha ukiwa umelewa Dawa za Kulevya

Dawa za kulevya, haramu na zilizoandikiwa na daktari, zinaweza kuathiri uwezo wako wa kuendesha gari kwa usalama. Ikiwa unaendesha gari ukiwa chini ya ushawishi wa dawa haramu au dawa zilizoandikwa na daktari za kulevya, unahatarisha usalama wako na wa watu wengine barabarani.

Polisi wa Victoria wanafanya upimaji wa dawa za kulevya bila kutarajia kote jimboni. Ukikutwa na dawa za kulevya mwilini mwako, utakabiliwa na adhabu kali.

Hakuna kiwango salama cha matumizi ya dawa wakati wa kuendesha gari. Matumizi ya dawa yoyote huambatana na hatari fulani.

### Unachoweza kufanya

Ikiwa una mpango wa kuendesha gari, chaguo salama zaidi ni kutokuwa na dawa za kulevya mwilini mwako.

## Vitu vya kuvuruga umakini (simu)

Simu za mkononi zinaweza kukuvuruga wakati unaendesha gari, jambo linaloongeza uwezekano wa kupata ajali mbaya.

Kuna sheria huko Victoria zinazobainisha jinsi unavyoweza kutumia simu ya mkononi au kifaa kingine wakati unaendesha gari, na kama unaweza kufanya hivyo.

Hakikisha unafahamu kanuni zinazohusu matumizi ya simu ya mkononi na vifaa vya kielektroniki kulingana na aina ya leseni yako. Unaweza kupata taarifa zaidi hapa:

(ingiza ukurasa wa tovuti baada ya kutafsiri)

Polisi wa Victoria na mtandao wa kamera za kugundua simu za mkononi hufanya kazi kote Victoria.

Ukikamatwa ukitumia simu yako ya mkononi kinyume cha sheria wakati unaendesha gari huko Victoria, utakabiliwa na adhabu kali: faini ya dola 627 na pointi 4 za adhabu.

### Unachoweza kufanya

- Ili kuepuka kuvurugwa na simu yako wakati unaendesha gari, tumia kipengele cha 'Usinisumbue' (Do Not Disturb) wakati wa kuendesha.
- Vinginevyo, weka simu yako katika hali ya kimya au iweke mahali ambapo huwezi kuifikia unapoendesha gari.
- Ikiwa kwa ujumla unapata ugumu wa kuzingatia unapoendesha gari, simama kando ya barabara kwa usalama na upumzike kutoka kwenye uendeshaji.



## Taarifa za ziada kuhusu usalama barabarani:

### Mikanda ya usalama

Kuvaa mkanda wa usalama kuna jukumu muhimu katika kuwalinda watu waliomo ndani ya gari iwapo kutatokea ajali au gari likisimama ghafla.

Ni sheria kwamba watu waliomo ndani ya gari, lori au basi lenye mikanda ya usalama lazima wavae mkanda huo.

Dereva wa gari lazima afunge mkanda wa usalama na kuhakikisha kuwa kila mtu ndani ya gari amefunga mkanda wake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na watoto.

Madereva wanaweza kutozwa faini ikiwa hawajafunga mkanda wa usalama au ikiwa abiria wao yeyote hajafunga mkanda wa usalama.

Abiria wenye umri wa miaka 16 na zaidi pia wanaweza kutozwa faini ikiwa hawatafunga mkanda wa usalama.

Kila mkanda wa usalama unaweza kutumiwa na mtu mmoja pekee. Hauwezi kuchangiwa. Taarifa zaidi kuhusu sheria za mikanda ya usalama zinapatikana hapa:

(ingiza tovuti baada ya kutafsiri)

Hivi ndivyo unavyoweza kuvaa mkanda wako wa usalama kwa usahihi:




Polisi wa Victoria na kamera za kugundua matumizi ya mikanda ya usalama zinafanya kazi kote Victoria.

**Ukikamatwa bila kufunga mkanda wa usalama au bila kuufunga ipasavyo, adhabu za sasa ni pointi 3 za makosa na faini ya $418 (kuanzia tarehe 1 Julai 2026).**

# Gharama ya kumiliki gari

## Mikopo

### Mikopo ya magari kutoka benki

Mikopo ya magari kutoka benki nchini Australia kwa kawaida hugawanywa katika makundi mawili:

- Mikopo yenye dhamana, inayotumia gari kama dhamana ili kupata riba ya chini
- Mikopo ya kibinafsi isiyo na dhamana, ambayo hutoa wepesi zaidi lakini ina viwango vya juu vya riba.

Benki nyingi kubwa hutoa mikopo ya magari yenye viwango vya riba visivyobadilika, na muda wa kurejesha kuanzia mwaka mmoja hadi saba.

Mikopo ya magari yenye dhamana: 7.49% kwa mwaka
Mikopo ya magari isiyo na dhamana 8.09% kwa mwaka
Kuna ada na gharama ambazo pia zinatozwa na Benki Kuu ya Australia.

### Watoa mikopo ya hadi siku ya malipo ya mshahara

Mkopo wa siku ya malipo (au mkopo wa kiasi kidogo) ni mkopo wa muda mfupi, usio na dhamana na wenye gharama kubwa.

Ingawa hutoa njia ya haraka ya kupata pesa kwa ajili ya dharura, mara nyingi huwa na ada za juu—hadi asilimia 20%

**NA**

Ada ya kila mwezi ya 4%—jambo linaloyafanya kuwa chaguo la gharama kubwa la kukopa linaloweza kusababisha mitego ya madeni.

*Kwa ujumla, njia mbadala kama vile malipo ya awali kutoka Centrelink, mikopo isiyo na riba (NILs), au mipango ya kifurushi cha mishahara hupendekezwa zaidi kuliko mikopo ya siku ya malipo.*



### Mkopo usio na riba kwa ajili ya magari

Ununuzi wa magari ya hadi dola 5,000 kwa matumizi muhimu.

Mikopo hii haina riba wala ada.
Sifa za kustahiki:
Pata kipato cha kila mwaka cha chini ya dola 70,000 (kabla ya kodi)

**AU** uwe na Kadi ya Huduma ya Afya/Kadi ya Pensheni

**AU** wamepitia ukatili wa kifamilia au wa nyumbani katika kipindi cha miaka 10 iliyopita

**NA** unaweza kuonyesha kuwa una uwezo wa kurejesha mkopo.

**Piga simu namba 1300 645 748 ili kufahamu kama unastahiki kuomba mkopo wa gari usio na riba.**

*Imetolewa na Good Shepherd Dandenong*

## Usajili wa Gari na Bima ya TAC ya Majeraha ya Kibinafsi huko Victoria

**Taarifa katika lugha mbalimbali kutoka VicRoads.**

**vicroads.vic.gov.au** Chagua lugha yako kwenye kona ya juu kulia ya skrini.

### Gharama za Usajili na Chaguzi za Malipo

Gharama za usajili wa magari hutofautiana kulingana na eneo na mzunguko wa malipo, huku maeneo ya miji mikubwa yakigharimu zaidi.

#### Umuhimu wa Kisheria wa Usajili

Kuendesha gari bila usajili kunaweza kusababisha faini na hatua za kisheria, jambo linalosisitiza umuhimu wa kuhuisha usajili kwa wakati.

### Kazi ya Bima ya TAC (Tume ya Ajali za Usafiri)

TAC hutoa bima ya lazima ya majeraha ya mtu wa tatu inayogharimia gharama za matibabu na ukarabati kutokana na ajali za usafiri.

TAC haigharamii uharibifu wa gari au mali, hivyo bima ya ziada inahitajika kwa ajili ya ulinzi kamili.

## Usajili na uhalali wa gari barabarani – Huduma ya Kisheria ya South-East Monash

### Usajili

Magari yote, kama vile magari ya kawaida, yanahitaji kusajiliwa ili kuendeshwa barabarani huko Victoria.

Lazima uende VicRoads kusajili gari lako; hapa ndipo mahali pale pale unapopaswa kwenda ili kupata leseni yako.

Unaweza kusajili gari kwa jina lako mwenyewe, lakini haliwezi kusajiliwa kwa zaidi ya mtu mmoja.

Usajili wako ukimalizika muda wake, huwezi kuendesha gari hilo.

Kuendesha gari lisilosajiliwa ni kinyume cha sheria.

### Cheti cha ustahiki wa gari barabarani:

Katika Victoria, gari linapouzwa au iwapo gari lililotumika linahitaji kusajiliwa upya, linahitaji Cheti cha Ustahiki wa Barabarani.

Ili kupata Cheti cha Ustahiki wa Barabarani, gari linahitaji kufanyiwa ukaguzi ili kuhakikisha kuwa sehemu zake muhimu zinafanya kazi vizuri na kwamba ni salama kuliendesha.

Gari kuwa na Cheti cha Ustahiki wa Barabarani (Roadworthy Certificate) haimaanishi kuwa gari hilo liko katika hali nzuri kabisa, au kwamba sehemu nyingine zisizohusiana na usalama (kwa mfano, mfumo wa kupoza hewa au vifutio vya vioo) zinafanya kazi.

### Tovuti ya Gari Yako Ni Salama Kiasi Gani

**howsafeisyourcar.com.au** ni nyenzo ya mtandaoni ya TAC inayowapa watumiaji taarifa huru kuhusu usalama wa magari. Tovuti hiyo inaonyesha taarifa za Mpango wa Tathmini ya Magari Mapya wa Australasia (ANCAP) na Viwango vya Usalama vya Magari Yaliyotumika (UCSR).

## Maandalizi ya leseni yako; mazoezi na kuweka nafasi ya kipimo - Huduma ya Kisheria ya South-East Monash

### Kipimo (mtihani) cha hatari

Wakati wa mtihani huo, utatazama video fupi 28 za sekunde 30 ambazo zinaonekana kana kwamba zimepigwa picha kutoka kwenye kiti cha dereva. Kwa kila video, lazima uonyeshe jinsi utakavyoitikia unapokuwa dereva. Kwa mfano, itabidi upunguze mwendo, upite gari lingine au usifanye lolote. Una dakika 45 za kumaliza mtihani, na unahitaji angalau asilimia 54 ili kufaulu.

### Jaribio la kuendesha gari

Ukishafaulu mtihani wa Maarifa ya Sheria na ule wa Kutambua Hatari, unaweza kujaribu kufanya mtihani wa kuendesha gari. Katika jaribio la kuendesha gari, ni lazima uonyeshe kuwa unaweza kuendesha kwa usalama, unaweza kulimudu gari vizuri, na unaweza kuzingatia sheria zote za barabarani pamoja na kuendesha kwa usalama huku ukiwa na magari mengine barabarani.

Afisa wa majaribio ya leseni kutoka VicRoads atakuwa ndani ya gari akikufanyisha mtihani huo. Ikiwa utafanya mtihani huo na mkufunzi wa udereva aliyehitimu kwa kutumia gari lenye mfumo wa udhibiti wa pande mbili, mkufunzi wa udereva atakaa kwenye kiti cha abiria. Ikiwa huendeshi gari ukiwa na mkufunzi wa kuendesha gari, hairuhusiwi kubeba mtu mwingine yeyote, kama vile rafiki.

Ikiwa unahitaji mkalimani, unaweza kuomba mmoja na VicRoads itamuandaa.

Huwezi kufanya mtihani wa kuendesha gari kwa kutumia aina yoyote ya gari, hivyo ni vyema kuhakikisha kuwa gari lako linafaa kwa ajili ya mtihani huo. Unaweza kupata taarifa hii kwenye tovuti ya VicRoads




*Tunawashukuru wale waliochangia katika nyenzo hii: Transport Accident Commission, Good Shepherd Dandenong, West Justice na South-East Monash Legal, pamoja na Kuanza Salama (Starting Out Safely) kwa kujumuisha nyenzo zao zilizotafsiriwa.*



# Kuendesha gari kwa Usalama katika Victoria

## Sheria muhimu za barabarani

**Lazima ufuate alama za trafiki barabarani.**

**Lazima ufuate taa za trafiki na ishara** na kuwa makini.

**Lazima ufuate masharti yote ya leseni yako** kama vile kuonyesha alama zako za "L" au "P" mbele na nyuma ya gari yako ikiwa una ruhusa ya kujifunza kuendesha au leseni ya Majaribio, kufuata vizuizi vya kubeba abiria, na vizuizi vya matumizi ya simu za mkononi.

**Lazima ufuate sheria ya kikomo cha kasi**.

**Lazima uvae mkanda wako wakati** unaendesha gari, na lazima uhakikishe kuwa umeuvaa kwa usahihi juu ya bega lako. **Lazima pia uhakikishe kuwa watu wote kwenye gari lako wamevaa mikanda yao** ya usalama kwa usahihi na uhakikishe kuwa watoto wamefungwa vizuri kwenye kiti sahihi cha gari kulingana na umri wao.

**Kuna sheria zinazokataza kuwa na pombe au dawa haramu mwilini mwako wakati wa kuendesha gari.** Kuna sheria tofauti kulingana na aina yako ya leseni. Kuvunja sheria hizi kunachukuliwa kwa ukali sana na polisi, mahakama na jamii. Inaweza kusababisha adhabu kubwa kama faini nzito, rekodi ya uhalifu, kufutwa kwa leseni na katika hali mbaya kifungo cha gerezani.

**Simu za mkononi**

Madereva wote wanapaswa kuwa na kifaa cha kushikia kwenye gari lao vifaa vyovyote vinavyobebeka kama simu za mkononi. Kuna adhabu kwa kutumia simu ya mkononi wakati wa kuendesha gari. Unaweza kupewa faini na kupunguzwa pointi 4 kwenye leseni yako ya udereva.

Kuna sheria tofauti kulingana na aina yako ya leseni. Hii inamaanisha ikiwa una kibali cha kujifunza, leseni ya majaribio au leseni kamili, unapaswa kujielimisha na sheria za leseni yako.

Kwa aina zote za leseni unapoendesha gari, hauwezi kutumia kifaa chako kuingiza habari (kwa mfano – Utafutaji kwenye Google au kutuma maandishi) au kuwa na kifaa chako kwenye mapaja yako au kuipatia kwa abiria.

Unaweza kuangalia matakwa haya yote na VicRoads kwenye https://www.vicroads.vic.gov.au/. Tovuti hii inaweza kutafsiriwa.




Westjustice



# Kuendesha gari kwa
## Usalama katika Victoria

### Adhabu

Ukikamatwa ukiwa umekiuka sheria za barabarani unaweza kupokea **faini au notisi ya ukiukaji** ambayo inakuomba ulipe pesa kufikia tarehe fulani.

Unaweza pia kupokea **pointi za upungufu** ambazo ni adhabu ambazo zimerekodiwa kwenye leseni yako ya kuendesha gari unapovunja sheria fulani za barabarani. Kwa mfano, kutovaa mkanda wako kwa usahihi, mwendo kasi, au kuingia kwenye makutanio ya barabara yenye taa nyekundu.

Kwa Leseni kamili ya Udereva (bluu) unaweza kupata pointi 11 tu za upungufu katika kipindi cha miaka mitatu. Kwa kibali cha Kujifunza (njano) au leseni ya majaribio (nyekundu au kijani) unaweza kupata pointi 4 tu za upungufu katika kipindi cha miezi 12, na huwezi kupata zaidi ya pointi 11 za upungufu katika kipindi cha miaka 3.
Ukivuka kikomo cha upungufu, VicRoads itakupa chaguzi mbili:

- Kusimamisha leseni yako mara moja kwa angalau miezi mitatu au zaidi;
- Unaweza kuchagua kuendelea kukaa na leseni yako na muda mrefu wa upungufu. Hii inamaanisha kwa miezi 12 haupaswi kufanya makosa yoyote ya upungufu. Ukipata hatua nyingine ya upungufu katika miezi 12, utapoteza leseni yako kwa muda mara mbili ya muda wa kusimamishwa mara moja.

Kama ukipokea taarifa ya **kusimamishwa kwa leseni au kukataliwa**, lazima usiendeshe gari hata kidogo. Utapewa ujumbe wa kusimamishwa kwa leseni au kukataliwa ikiwa:

- umeenda juu ya mipaka ya pointi za upungufu za leseni yako;
- umeendesha 25 km/h au zaidi juu ya kikomo cha kasi, au 130 km/h au zaidi katika eneo la kikomo cha kasi cha 110 km/h.
- umekamatwa ukiendesha gari ukiwa umekunywa pombe au kuendesha gari ukiwa umutumia dawa za kulevya.

Hii sio orodha yote kamili ya jinsi leseni yako inaweza kusimamishwa au kufutwa.

Ikiwa leseni yako imesimamishwa kwa sababu ya kuendesha gari ukiwa umekunywa na kuendesha gari ukiwa umetumia dawa za kulevya, itabidi ufanye kazi kadhaa kabla ya kurejeshewa leseni yako, pamoja na:

- Kukamilisha programu ya elimu kuhusu kubadilisha tabia yako ya kuendesha gari;
- Kusakinisha kifaa kwenye gari lako ambacho unapaswa kupuliza kabla ya gari lako kuanza kuthibitisha kuwa haujakunywa pombe (' interlock device').

Kuna adhabu kali kwa kuendesha gari wakati umesimamishwa au kukataliwa katika Victoria.

Kwa ushauri wa kisheria wa bure na wa siri tafadhali wasiliana nasi:

(03) 9749 7720
admin@westjustice.org.au

Westjustice



# Kuelewa Bima

Bima ni kitu unachonunua ili kukukinga dhidi ya kulipa gharama kamili ikiwa kitu kisichotarajiwa kitatokea kama ajali, ugonjwa au wizi.

Unaponunua bima ya gari, unakubali kulipa ada ya kampuni, na kwa kurudi wanaweza kupunguza au kulipa gharama ya hasara unayopata. Bima haikingi hatari zote au aina zote za hasara.

Ikiwa una ajali ya gari na huna bima, unaweza kulipia uharibifu wote uliyosababisha katika ajali.

## Bima unayopata moja kwa moja unaposajili gari lako

### Bima ya Majeraha ya Kibinafsi - Tume ya Ajali ya Usafiri

Unaposajili gari lako katika Victoria, gharama ya usajili wa gari inajumuisha bima kwa majeraha uliyosababisha na ajali ya gari. Inaitwa 'gharama za Tume ya Ajali ya Usafiri'. Bima hii inashughulikia gharama ya bili za matibabu ikiwa umejeruhiwa katika ajali ya gari, na kwa kupoteza mapato ikiwa huwezi kufanya kazi kwa sababu ya ajali ya gari.

Ikiwa umejeruhiwa kimwili au kisaikolojia, madai kwa Tume ya Ajali ya Usafiri (Transport Accident Commission (TAC)) lazima yafanywe ndani ya miezi 12 tangu tarehe ya ajali, au miezi 12 kutoka tarehe ambayo jeraha lako kutokana na ajali ya gari linakuwa wazi.

## Bima unayopaswa kununua kutoka kwa kampuni ya bima

Maelezo ya bima yako yatakuwa katika hati inayoitwa Taarifa ya Ufichuzi wa Bidhaa na Ratiba ya Sera ambayo bima yako itakupa. Unapotoa dai juu ya bima yako unaweza kulipa ada inayoitwa 'ziada (excess).'

### Bima ya Uharibifu wa Mali ya Mtu wa Tatu au Uharibifu wa Mali ya Mtu wa Tatu, Bima ya Moto na Wizi

Bima ya Uharibifu wa Mali ya Wahusika Wengine inashughulikia gharama ya uharibifu unaosababisha kwa gari la mtu mwingine au kwa mali ya mtu mwingine (kama uzio au nyumba). Ikiwa inajumuisha bima ya moto na wizi, inaweza pia kulipia gharama hadi kiasi fulani ikiwa gari lako limeibiwa au kuharibiwa na wizi, au ikiwa gari lako limeharibiwa na moto. Haitoi gharama ya uharibifu unaosababisha kwa gari lako mwenyewe katika ajali.

Bima hii ni ya hiari, ambayo ina maana kwamba unapaswa kununua kando na usajili wa gari lako.

Wakati dereva mwingine ana makosa na hana bima, unaweza kupata bima ya Ugani wa Magari Isiyo na Bima (Uninsured Motorist Extension (UME)) chini ya sera ya Bima ya Mali ya Mtu wa Tatu.

Westjustice



# Kuelewa Bima

## Bima ya Uharibifu wa Mali ya Kina

Bima hii inashughulikia gharama ya uharibifu unaosababisha katika ajali ya gari au mali ya mtu mwingine (kama uzio au nyumba) na uharibifu unaosababishwa na gari lako. Pia inashughulikia gharama ikiwa gari lako limeibiwa au kuharibiwa na wizi na ikiwa limeharibiwa na moto.

Maelezo kuhusu kiasi gani bima yako italipa yatakuwa katika hati inayoitwa Taarifa ya Ufichuzi wa Bidhaa na Ratiba ya Sera ambayo bima yako itakupa. Bima hii ni ya hiari ambayo inamaanisha lazima ununue kando na usajili wa gari lako.

## Nini cha kufanya ikiwa umepata ajali ya gari

- Lazima usimamishe gari lako mahali salama na uangalie ikiwa kuna mtu yeyote amejeruhiwa. Ni kinyume na sheria ikiwa utaendelea kuendesha gari na kushindwa kusimama.
- Ikiwa mtu amejeruhiwa piga simu 000 na uombe Polisi na Ambulensi waje mahali ulipo.
- Lazima umpe dereva mwingine na mtu yeyote aliyejeruhiwa jina lako, anwani, na nambari ya usajili wa gari. Ikiwa mtu mwingine anamiliki gari ulilokuwa ukiendesha, unapaswa kutoa maelezo yake ya kibinafsi. Ingawa haihitajiki na sheria, ni vizuri kuuliza nambari ya simu na maelezo ya kampuni ya bima.
- Unapaswa kumuuliza dereva mwingine, au mashahidi wowote kwa jina lao, anwani na nambari ya usajili wa gari. Ingawa haihitajiki na sheria, ni vizuri pia kubadilishana nambari za simu na maelezo ya kampuni ya bima.
- Angalia ikiwa gari lako, gari lingine lolote lililohusika katika ajali, au mali yoyote ya kibinafsi katika eneo la ajali imeharibiwa. Piga picha za uharibifu uliosababishwa kwenye magari au mali nyingine yoyote (ikiwa ni salama kufanya hivyo).
- Ikiwa Polisi watakuja kwenye ajali, wape maelezo yako ya kibinafsi na ueleze kilichotokea . Ikiwa dereva mwingine hatakupa maelezo yake ya kibinafsi, ripoti hii kwa Polisi.
- Usikubali kosa ambalo hukulifanya usikubali kwamba ulifanya kitu kibaya na kusababisha ajali.
- Andika kile kilichotokea, jinsi na wapi ajali ilitokea.
- Iambie kampuni yako ya bima kuhusu ajali haraka iwezekanavyo.

Kwa ushauri wa kisheria wa bure na wa siri tafadhali wasiliana nasi:

(03) 9749 7720
admin@westjustice.org.au
Westjustice